Kikao kilipokea taarifa hiyo na kusisitiza kuwa hoja zote ambazo bado hazijafungwa zijibiwe kwa wakati ili Mkaguzi aweze kuhakiki majibu ya hoja hizo na kuweza kufunga hoja husika.

**DO.NA.79/FUM.07/2021/2022 - TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA KITENGO CHA TEHAMA KWA ROBO YA PILI KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022**

Kaimu Afisa TEHAMA aliwasilisha kwenye kikao taarifa ya Kitengo hicho ambapo kinasimamia mifumo mbalimbali kama vile mfumo wa makusanyo ya mapato ya ndani, mfumo wa malipo, mfumo wa utumishi, mfumo wa ulipaji mishahara kwa watumishi wa umma, mfumo wa malipo na matumizi kwa ajili ya shule, vituo vya afya, zahanati na hospitali, mfumo kwa ajili ya takwimu za kielimu, mfumo kwa ajili ya matibabu, mfumo kwa ajili ya malipo ya Serikali, mfumo wa kodi za ardhi, mfumo kwa ajili ya bajeti, mfumo wa taarifa za shule, mfumo wa manunuzi ya umma, mfumo wa ugawaji wa vitambulisho kwa wajasiliamali wadogo, mfumo kwa ajili ya kusajili wanachama wa afya ya jamii, mfumo wa taarifa kwa shule za sekondari na mfumo wa taarifa kwa shule za msingi. Aidha, kuliwasilishwa taarifa inayohusiana na habari ambapo Halmashauri hutoa taarifa mbalimbali kwa wananchi kutumia redio, runinga, magazeti na mitandao ya kijamii.

Kikao kilipokea taarifa hiyo, kilijadili na kuipitisha.

**DO.NA.80/FUM.07/2021/2022 - OMBI LA KUINGIZA BAJETI YA NYONGEZA (SUPPLEMENTARY BUDGET) TSHS: 91,520,000.00 KUTOKA SHIRIKA LINALOHUDUMIA WATOTO DUNIANI (UNICEF) KWA AJILI YA UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZINAZOFADHILIWA NA SHIRIKA HILO**

Kaimu Afisa Mipango Wilaya aliwasilisha kwenye kikao ombi la kuingiza bajeti ya nyongeza (supplementary budget) ya Tshs: 91,520,000.00 kutoka shirika linalohudumia Watoto Duniani (UNICEF) kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli zinazofadhiliwa na shirika hilo kwenye mfumo wa "PLANREP" na "FFARS" ili fedha hizo ziweze kutumika kwa makusudi tarajiwa. Ilielezwa kuwa Idara ya Elimu Msingi ilipokea fedha kutoka UNICEF kiasi cha Tshs: 91,520,000.00 kwa ajili ya kutekeleza mafunzo kwa Walimu Wakuu, Walimu na Kamati za shule kwa ajili ya kuwajengea uwezo wanafunzi wa kike kupitia programu ya Sara Redio (SRP).

Kikao kilipokea taarifa hiyo, kiliridhia utanuzi wa vifungu na kupitisha.

**DO.NA.81/FUM.07/2021/2022 - MAPOKEZI YA FEDHA KWA AJILI YA MIRADI YA IDARA YA AFYA KUTOKA SERIKALI KUU PAMOJA NA MAOMBI YA KUTANUA VIFUNGU VYA MATUMIZI YA FEDHA HIZO**

Kaimu Afisa Mipango Wilaya aliwasilisha kwenye kikao taarifa ya mapokezi ya fedha kwa ajili ya miradi ya Idara ya afya kutoka Serikali Kuu kwa mchanganuo ufuatao:-



Scanned with CamScanner

| NA | JINA LA MRADI | KIASI CHA FEDHA |
|---|---|---|
| 1 | Ukarabati wa miundombinu ya hospitali ya Wilaya ya Tukuyu (Makandana) | 1,000,000,000.00 |
| | Ujenzi wa jengo la dharura la nje (EMD) katika hospitali ya Wilaya ya Tukuyu | 300,000,000.00 |
| | Ujenzi wa nyumba ya watumishi (Three in one) kituo cha afya cha Kyimo | 90,000,000.00 |
| 2 | Ukamilishaji wa zahanati ya Isyonje | 50,000,000.00 |
| 3 | Ukamilishaji wa zahanati ya Ilenge | 50,000,000.00 |
| 4 | Ukamilishaji wa kituo cha afya cha Mpuguso | 50,000,000.00 |
| 5 | Ujenzi wa kituo cha afya cha Iponjola | 500,000,000.00 |
| 6 | **Jumla** | **2,040,000,000.00** |

Aidha, alieleza kuwa kwa upande wa jengo la wagonjwa wa dharura wa nje pamoja na jengo la watumishi (three in one), awali majengo hayo mawili TAMISEMI waliagiza yajengwe kwa kutumia wakandarasi badala ya kutumia "local fundi" lakini baada ya Halmashauri zote kuwasilisha gharama walizoainisha wakandarasi kwa TAMISEMI kuonekana kuwa juu kwa mfano zaidi ya Tshs: 550,000,000.00 kwa jengo la dharura na zaidi ya Tshs: 145,000,000.00 kwa nyumba za watumishi. Hivyo, ilielezwa kuwa TAMISEMI ilitoa mabadiliko kwa barua yenye kumbukumbu namba AH.161/298/01 ya tarehe 13/01/2022, ikiagiza kwamba ujenzi wa majengo hayo utumike mfumo wa "Force account".

Pia, alieleza kuwa miongoni mwa fedha zilizopokelewa kiasi cha Tshs: 1,040,000,000.00 ni kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha afya cha Iponjola, ukamilishaji wa zahanati za Isyonje na Ilenge, upanuzi wa miundombinu katika kituo cha afya cha Mpuguso, ujenzi wa jengo la dharura katika hospitali ya Wilaya ya Tukuyu pamoja na ujenzi wa nyumba ya watumishi katika kituo cha afya cha Kyimo. Alieleza kuwa inaombwa idhini ya kutanua vifungu kwenye mfumo wa FFARS ili fedha hiyo iweze kuwa tayari kwa matumizi.

Kikao kilipokea taarifa hiyo, kiliridhia kutanua vifungu na kutoa maoni kama ifuatavyo:-

- Pongezi zilitolewa Serikali Kuu kwa kutoa fedha kwa ajili ya ukarabati na ujenzi katika hospitali ya Wilaya ya Tukuyu (Makandana).
- Wajumbe walishauri kuwa utekelezaji wa miradi hiyo uendane na uhalisia wa fedha zilizotolewa na Serikali ili kuwezesha kuwa na hospitali nzuri ya Wilaya.
- Ilielezwa kuwa hali ya utoaji wa huduma katika hospitali ya Wilaya ya Tukuyu hairidhishi hivyo Mkurugenzi Mtendaji Wilaya aliangalie suala hilo kwa undani zaidi, Katibu alitoa ufafanuzi kuwa tayari walishaanza kuchukua hatua kwa kero zinazojitokeza katika hospitali hiyo na zoezi hilo ni endelevu kwa wale wote wanaobainika kutofuata misingi ya utoaji wa huduma ya afya kwenye hospitali hiyo watachukuliwa hatua stahiki



Scanned with CamScanner

**DO.NA.82/FUM.07/2021/2022 – KUFUNGA KIKAO**

Katibu alimkaribisha Mwenyekiti kwa ajili ya kufunga kikao. Mwenyekiti aliwashukuru wajumbe kwa michango yao ya mawazo kwa hoja zilizowasilishwa katika kikao hicho na aliwakumbusha Wakuu wa Idara na Vitengo kutekeleza maagizo yote yaliyotolewa katika kikao. Aidha, alisisitiza kuwa suala la ujenzi wa mabweni kwa wanafunzi wa sekondari lianze kupangwa katika mipango ya Halmashauri. Pia, alikumbusha kuwa wananchi waendelee kuhamasishwa kuwa na vyoo bora katika makazi yao. Sambamaba na hayo alieleza kuwa suala la udumavu kwa watoto linatakiwa kufanyiwa kazi kwa sababu Kiwilaya kuna 23% hivyo suala la lishe bora linatakiwa kuhamasishwa katika jamii ili kupunguza tatizo hilo katika Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe. Kisha alifunga kikao saa 09:22 Alasiri.

**MUHTASARI UMETHIBITISHWA NA:-**

| | |
|---|---|
| ........................................ | ........................................ |
| **MHE: SAMWEL MWINUKA** | **BW: CASTORY MAKEULA** |
| **MWENYEKITI** | **KATIBU** |

**TAREHE** 24/02/2022



Scanned with CamScanner

**MUHTASARI WA KIKAO CHA KAMATI YA FEDHA, UONGOZI NA MIPANGO CHA TAREHE 31/01/2022, KILICHOFANYIKA KATIKA UKUMBI WA HALMASHAURI YA WILAYA YA RUNGWE WA JOHN A. MWANKENJA**

**WALIOHUDHURIA**

**A: WAJUMBE**

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Mhe: Samwel Mwinuka | Diwani Kata ya Ndanto | Mwenyekiti |
| 2. | Mhe: Moyo Mbamba | Diwani Kata ya Iponjola | Mjumbe |
| 3. | Mhe. Samwel Mwakasege | Diwani Kata ya Matwebe | Mjumbe |
| 4. | Mhe: Abraham Mwankenja | Diwani Kata ya Bujela | Mjumbe |
| 5. | Mhe: Lydia Sanga | Diwani Kata ya Ibighi | Mjumbe |
| 6. | Mhe: Emmy Maseta | Diwani V/M Kata ya Kyimo | Mjumbe |
| 7. | Mhe: Saimon Kabuje | Diwani Kata ya Bagamoyo | Mjumbe |
| 8 | Mhe: Salome Mwakapala | Diwani V/M Kata ya Msasani | Mjumbe |

**B: WASIOHUDHURIA**

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Mhe: Antony Mwantona | Mbunge Jimbo la Rungwe | – Kwa taarifa |
| 2. | Mhe: Mpokigwa Mwankuga | Diwani Kata ya Masoko | – Kwa taarifa |

**C: WATENDAJI**

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Bw: Castory Makeula | Kaimu Mkurugenzi Mtendaji (W) – Katibu |
| 2. | Bw: Liston Mbughi | Kaimu Afisa Utumishi (W) |
| 3. | Bw: Noah Sikwese | Kaimu Afisa Mipango (W) |
| 4. | Bw: Victor Mwakapala | Afisa Manunuzi (W) |
| 5. | Bw: Augustino Lawi | Afisa Mifugo na Uvuvi (W) |
| 6. | Bw: Stephen Mbiza | Kaimu Afisa Kilimo,Umwagiliaji na Ushirika (W) |
| 7. | Eng: Anosisye Mwasege | Kaimu Mhandisi wa Ujenzi (W) |
| 8. | Bw: Salum Kilanga | Kaimu Afisa Usafi na Mazingira (W) |
| 9. | Bw: Omary Mungi | Afisa Maendeleo ya Jamii (W) |
| 10. | Bibi: Lyidia Mwakatumbula | Mratibu wa TASAF (W) |
| 11. | Bw: Meritus Menshi | Afisa Biashara (W) |
| 12. | Bw: Lucas Ndombele | Mweka Hazina (W) |
| 13. | Bibi: Edda Shimwela | Kaimu Afisa TEHAMA (W) |
| 14. | Bw: Isaya Kitumbika | Kny: Mganga Mkuu (W) |
| 15. | Mwl. Gerald Kifyasi | Afisa Elimu Msingi (W) |
| 16. | Mwl. Hyera Auckland | Kaimu Afisa Elimu Sekondari (W) |
| 17. | Bw: Simon Mutabazi | Kaimu Mkaguzi wa Ndani (W) |
| 18. | Bw: Emmanuel Mwakiwone | Afisa Mapato |
| 19. | Bibi: Janeth Chang'a | Kaimu Mwanasheria wa Halmashauri |
| 20. | Bibi: Emiliana Chammy | Kny: Afisa Ardhi na Maliasili (W) |
| 21. | Bw: Christopher Nyambaza | Kaimu Afisa Uchaguzi (W) |
| 22. | Bw: Deogratus Mwaigaga | Kaimu Afisa Mtendaji wa Mamlaka ya Mji |



Scanned with CamScanner